# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA SAYANSI NA TECKNOLOGJIA
**KWA ELIMU YA MAANDALIZI ZANZIBAR**

**TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR**

**2012**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2012

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, maandishi nukta nundu na kutoa Muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Zanzibar
S.L.P. 840
**Zanzibar**

# YALIYOMO

Ukurasa

YALIYOMO ........ ii

Utangulizi ........ iii

Ujuzi wa Jumla katika Somo la Elimu ya mazingira Sayansi na Teknolojia ........ iii

Malengo ya Jumla ya Somo la Elimu ya Mazingira Sayansi na Teknolojia ........ iv

MUHTASARI WA SAYANSI MWAKA WA KWANZA ........ 1

MWAKA WA PILI ........ 17

# Utangulizi

Katika hatua za awali za ukuaji wa mtoto Elimu ya Mazingira, Sayansi na Teknolojia ni muhimu sana kwani inamfanya mtoto kuwa mchunguzi, mdadisi, mvumbuzi na kuanza kupata uwezo wa kuchunguza kisayansi. Mtoto hujifunza jinsi ya kujitambua mwenyewe na kuyajua mambo mengi yanayomzunguka. Aidha mtoto hujifunza Elimu ya Mazingira, Sayansi na Teknolojia kupitia michezo ili aweze kuyapenda, kuyatumia, kuyathamini na kuyatunza mazingira yaliyomzunguka.

## Ujuzi wa Jumla katika Somo la Elimu ya mazingira Sayansi na Teknolojia

Baada ya kusoma somo la Elimu ya Mazingira, Sayansi na Teknolojia katika skuli za Maandalizi, watoto wataonesha ujuzi wa:-

1. Kuelezea uhusiano wa kifamilia, ujirani na kijamii pamoja na mgawanyo wa majukumu katika familia na jamii.
2. Kuvuta, kusukuma na kuchunguza kani (nguvu) za vitu mbali mbali pamoja na kuainisha vitu vinavyoelea na kuzama.
3. Kuelezea maumbile ya dunia yetu na mabadiliko ya hali ya hewa.
4. Kuainisha njia za mawasiliano za kale na za sasa.
5. Kutumia stadi za kujifunza sayansi.
6. Kutunza afya zao kwa kudumisha usafi wa kiwiliwili, mazingira yanayowazunguka na kutumia lishe bora ili kuepukana na maradhi.
7. Kuelezea mazingira yanayotishia usalama wao yakiwemo yale yanayopelekea maambukizi ya virusi vya UKUMWI na utumiaji wa dawa za kulevya na njia za kujikinga.
8. Kuainisha aina za majengo mbali mbali na matumizi yake katika jamii.
9. Kutumia milango mitano ya ufahamu.
10. Kuchunguza na kudadisi mazingira yaliyomzunguka.

**Malengo ya Jumla ya Somo la Elimu ya Mazingira Sayansi na Teknolojia**

Somo la Elimu ya Mazingira, Sayansi na Teknolojia linafundishwa katika skuli za Maandalizi ili watoto waweze:-

1. Kuelewa uainishaji wa vitu vyenye uhai na visivyo na uhai.
2. Kupata stadi za kujifunza Sayansi.
3. Kutambua uhusiano na umuhimu wa kifamilia, ujirani na kijamii pamoja na mgawanyo wa majukumu katika familia na jamii.
4. Kupata uzoefu wa uvutaji, usukumaji na uchunguzi wa kani (nguvu) za vitu mbali mbali pamoja na uainishaji wa vitu vinavyoelea na kuzama.
5. Kutambua maumbile ya dunia yetu na mabadiliko ya hali ya hewa.
6. Kuzitambua njia za mawasiliano za kale na za sasa.
7. Kujenga tabia ya utunzaji wa afya zao kwa kudumisha usafi wa kiwiliwili, mazingira yanayowazunguka na kutumia lishe bora ili kuepukana na maradhi.
8. Kutambua mazingira yanayotishia usalama wao yakiwemo yale yanayopelekea maambukizi ya virusi vya UKIMWI na utumiaji wa dawa za kulevya na jinsi ya kujikinga.
9. Kutambua majengo mbali mbali na matumizi yake katika jamii.
10. Kutambua matumizi ya milango mitano ya fahamu.
11. Kujenga uzoefu wa uchunguzi na udadisi wa mazingira yaliyomzunguka.

# MUHTASARI WA SAYANSI MWAKA WA KWANZA

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. FAMILIA<br>Uhusiano wa Watu katika Familia. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja watu anaokaa nao nyumbani | Kwa kutumia mbinu ya masuali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja watu anaokaa nao nyumbani | 1. Chati inayoonesha watu waliomo katika familia mf. Baba, mama, bibi, babu, kaka dada.<br>2. Picha mguso inayoonesha watu walio katika familia. | 6 |
| | (ii) Kuelezea uhusiano wao. | 1. Kwa kutumia mbinu ya masuali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza uhusiano wao<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kuchora mwalimu awaongoze watoto kuchora picha ya mtu yeyote katika familia. | 1. Chati inayoonesha watu waliomo katika familia mf. Babu, kaka dada.<br>2. Picha mguso inayoonesha watu walio katika familia Baba, mama, bibi, | |
| 2. VIUMBE VYENYE UHAI NA VITU VISIVYO NA UHAI<br>(a) Vitu Vyenye Uhai. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja mifano ya viumbe vyenye uhai. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kuainisha viumbe vyenye uhai vilioko katika mazingira yao.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya ziara mwalimu awaongoze watoto kutembelea sehemu zenye wanyama, ndege, miti, wadudu. | 1. Vitu halisi mf ng’ombe, punda, farasi, miti, ndege.<br>2. Chati ya vitu vyenye uhai.<br>3. Chati mguso. Ya vitu vyenye uhai | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | 3. Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora viumbe vyenye uhai. | | |
| | (ii) Kueleza sifa za viumbe vyenye uhai | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kuchunguza na kutaja sifa za viumbe vyenye uhai | 1. Vitu halisi mf ng'ombe | |
| | | . | punda, farasi, miti, ndege.<br>2. Chati ya vitu vyenye uhai.<br>3. Modeli za vitu vyenye uhai<br>4. Chati mguso ya vitu vyenye uhai | |
| (b) Vitu visivyo na Uhai | Mtoto aweze:-<br>(I) Kutaja vitu visivyo na uhai | Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kutaja vitu visivyo na uhai. | 1. Vifaa halisi mf. Kiti, meza, mawe, vibao, gari.<br>2. Chati ya vitu visivyo na uhai/chati mguso ya vitu visivyo na uhai. | 6 |
| | (ii) Kutaja sifa za vitu visivyo na uhai. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja sifa za vitu visivyo na uhai | 1. Vifaa halisi mf. Kiti, meza, mawe, vibao, gari n.k.<br>2. Chati ya vitu visivyo na uhai/chati | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | mguso ya vitu visivyo na uhai. | |
| | (iii) Kutofautisha sifa za viumbe vyenye uhai na vitu visivyo na uhai | Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kutofautisha viumbe vyenye uhai na vitu visivyo na uhai. | 1. Vifaa halisi mf. Kiti, meza, mawe, vibao, gari n.k.<br>2. Chati ya viumbe visivyo na uhai/chati mguso ya vitu visivyo na uhai. | |
| . 3. NGUVU ZA MAUMBILE.<br>(a) Vitu Vinavyoelea | Mtoto aweze:-<br>(i) Kufanya jaribio la vitu vinavyoelea. | Kwa kutumia mbinu ya jaribio mwalimu awaongoze watoto kuingiza vitu katika maji. | 1. Beseni la maji<br>2. Ngarawa za karatasi<br>3. Chupa ya plastic<br>4. Gamba la buyu<br>5. Kibakuli cha plastiki | 3 |
| | (ii) Kuainisha vitu vinavyoelea | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya vitu vinavyoelea na kueleza sababu za vitu kuelea. | 1. Beseni lenye maji.<br>2. Ngarawa za karatasi<br>3. Chupa ya plastiki<br>4. Gamba la buyu.<br>.5. Kibakuli cha plastiki | |
| | (III) Kueleza sababu za vitu kuelea | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto | 1. Beseni lenye maji.<br>2. Ngarawa za karatasi | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kueleza sababu za vitu kuelea | 3. Chupa ya plastiki<br>4. Gamba la buyu. | |
| (b) Vitu Vinavyozama | Mtoto aweze:-<br>(i) Kufanya jaribio la vitu vinavyozama. | 1. Kwa kutumia mbinu ya jaribio mwalimu awaongoze watoto kutia vitu mbali mbali katika maji. | 1. Beseni la maji.<br>2. Mawe,<br>3. Vipande vya chuma.<br>4. Sarafu na Kibao. | 3 |
| | (ii) Kutaja vitu vinavyozama | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja vitu vinavyozama. | 1. Beseni la maji.<br>2. Mawe,<br>3. Vipande vya chuma.<br>4. Sarafu na Kibao. | |
| | (iii) Kueleza sababu ya vitu kuzama | Kwa kutumia mbinu ya hadithi mwalimu awaongoze watoto kutoa sababu za kuzama. | 1. Beseni la maji.<br>2. Mawe,<br>3. Vipande vya chuma.<br>5. Sarafu na | |
| 4. ZANZIBAR<br>(a) Visiwa cha | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuelezea | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto | 1. Ramani ya Visiwa vya Zanzibar. | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Unguja na Pemba. | maumbile ya Zanzibar. | kutaja jina la nchi yetu. | 2. Radio,<br>3. Kaseti.<br>4. CD.<br>5. | |
| | (ii) Kutafautisha ramani ya kisiwa cha Unguja na Pemba. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo (Nchi yetu Zanzibar) mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo ya Nchi yetu Zanzibar..<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kutafautisha ramani za visiwa vya Unguja na Pemba | 1. Ramani ya Visiwa vya Zanzibar.<br>1. Radio,<br>2. Kaseti.<br>4. CD. | |
| 5.MAWASILIANO<br>(a) Mawasiliano ya Kale. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kueleza namna ya watu wa kale walivyokuwa wakiwasiliana | Kwa kutumia mbinu ya hadithi mwalimu awaongoze watoto kuelezea namna ya watu wa kale walivyokuwa wakiwasiliana. | 1. Vitabu.<br>2. Chati/chati mguso.<br>3. Sinema boksi 4. Ngoma.<br>5. Pembe<br>6. Upatu na barua. | 3 |
| (b) Mawasiliano ya Sasa | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutumia njia za mawasiliano ya kisasa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kutaja vitu vinavyotumika katika mawasiliano ya sasa. | 1. Simu.<br>2. Kompyuta.<br>3. Intaneti.<br>4. Redio. | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza matumizi ya vitu vya mawasiliano ya sasa<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mchoro | 5. TV.<br>6. Mod vya mawasiliano ya kisasa.eli ya vitu<br>7. Chati ya vitu vya mawasiliano ya kisasa/chati mguso | |
| | | .<br>mwalimu awaongoze watoto kuchora vitu vya mawasiliano ya sasa. | | |
| 6. USAFIRI<br>(a) Usafiri wa Kale | Mtoto aweze:<br>(i) Kueleza namna ya watu wa kale walivyokuwa wakisafiri. | Kwa kutumia mbinu hadithi mwalimu awaongoze watoto kuelezea namna ya watu wa kale walivyokuwa wakisafiri. | 1. Vitabu.<br>2. Chati yenye kuonesha usafiri wa kale/chati mguso. | 3 |
| | (ii) Kutofautisha njia za mawasiliano za kisasa na za kale. | Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kutofautisha njia za mawasiliano za kale na za sasa. | 1. Simu.<br>2. Kompyuta.<br>3. Intaneti.<br>4. Redio.<br>5. TV.<br>6. Modeli ya vitu vya mawasiliano ya | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | kisasa.<br>7. Chati ya vitu vya mawasiliano ya kisasa/chati mguso | |
| (b) Usafiri wa sasa. | Mtoto aweze:-<br>Kuelezea njia za usafiri za kisasa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya ziara mwalimu awapeleke watoto sehemu watakazoona vyombo vya usafiri wa kisasa.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kutazama filamu na kuelezea matumizi ya vyombo vya usafiri wa kisasa.<br>3 Kwa mbinu ya kuchora/kupaka rangi mwalimu awongoze watoto kuchora vyombo vya usafiri wa angani, nchi kavu, baharini. | 1. Vyombo vya usafiri wa angani, nchi kavu, baharini.<br>2. T.V.<br>3. CD.<br>4. DVD | 3 |
| 6. AFYA NA MARADHI<br>(a) Usafi wa Mwili. | Mtoto aweze:- kupiga mswaki, kukata kucha, kuchana nywele, kukoga, kuvaa nguo safi. | . Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kuigiza namna ya kupiga mswaki, kukata kucha, kuchana nywele, kukoga, kuvaa nguo<br>safi | 1. Vifaa halisi.<br>2. Mswaki.<br>3. Ndoo yenye maji<br>4. Sabuni<br>5. Dawa ya meno<br>6. Pasi | 12 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | 7. Mafuta.<br>8. Chati inayoonesha vitu vinavyotumika katika utunzaji wa afya. | |
| (b) Usafi wa Mazingira | Mtoto aweze kusafisha mazingira anayoishi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea namna ya kusafisha mazingira anayoishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kuigiza namna ya kusafisha mazingira mfano kufagia , kuzoa taka, kuokota taka. | 1. Ufagio, kizoleo, debe la taka.<br>2. Chati ya vifaa vya kufanyia usafi.<br>3. Chati inayoonesha watoto wanafanya usafi/chati mguso. | 6 |
| (c) Maradhi yanayowasumbua watoto<br>- Malaria<br>- Kuharisha | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja maradhi yanayowasumbua. watoto. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja maradhi yanayowasumbua. | 1. Chati ya watoto wanaosumbuliwa na maradhi/chati mguso.<br>2. Modeli ya kitanda na chandarua. | 6 |
| | (ii) Kueleza sababu za maradhi yanayowasumbua watoto. | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kueleza maradhi yanayowasumbua na sababu za maradhi hayo | 1. Chati ya watoto wanaosumbuliwa na maradhi/chati mguso.<br>2. Modeli ya kitanda na chandarua. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 8. CHAKULA NA LISHE<br>(a) Majina ya Vyakula | Mtoto aweze kutaja majina ya vyakula. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya vyakula.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kutofautisha aina za vyakula. | 1. Vyakula halisi.<br>2. Chati ya vyakula mbali mbali/chati mguso. | 6 |
| (b) Makundi ya Vyakula | Mttoto aweze kupanga makundi ya vyakula. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo ya makundi ya vyakula.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya michezo mwalimu awaongoze watoto kupanga makundi ya vyakula. | 1. Vyakula halisi.<br>2. Chati ya vyakula mbali mbali/chati mguso.<br>3. Chati ya nyimmbo/chati mguso | |
| (c) Mlo kamili | Mtoto aweze kuelezea mlo kamili | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuelezea mlo kamili. | 1. Chati za nyimbo/nukta nundu | |
| 9. DAWA ZA KULEVYA<br>(a) Aina za Dawa za Kulevya. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja aina za dawa za kulevya. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja aina za dawa za kulevya.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kuangalia filamu inayoonesha | 1. Picha za waathirika na dawa za kulevya.<br>2. Video.<br>3. CD.<br>4. T.V. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | waathirika wa dawa za kulevya.na aina za dawa za kulevya. | | |
| | (ii) Kuelezea athari za dawa za kulevya. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza athari za dawa za kulevya. | 1. Picha za waathirika na dawa za kulevya.<br>2. Video.<br>3. CD.<br>4. T.V.<br>5. | |
| 9. V.V.U NA UKIMWI<br><br>(a) Maambukizi ya V.V.U. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja vitu Vinavyoweza kuambukiza virusi vya UKIMWI | Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto<br>kuvitaja vitu vinavyoweza kuambukiza V.V.U | 1. Bomba la sindano.<br>2. Sindano ya kushonea.<br>3. Kiwembe.<br>4. Kampasi.<br>5. Vitu vyenye ncha kali.<br>6. Mate.<br>7. Mabofu.<br>8. Picha inayoonesha mchuruziko wa damu na mtoto anamtumbua mwenziwe jipu au kipele. | 6 |
| | (ii) Kuelezea namna | Kwa kutumia mbinu ya maswali na | 1. Bomba la sindano | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | mtoto anavyoweza kuambukizwa V.V.U | majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea namna mtoto anavyoweza kuambukizwa V.V.U. | 2. Sindano ya kushonea.<br>3. Kiwembe.<br>4. Kampasi.<br>5. Vitu vyenye ncha kali.<br>6. Mate.<br>7. Mabofu.<br>8. Picha inayoonesha mchuruziko wa damu na mtoto anamtumbua mwenziwe jipu au kipele. | |
| | (iii) Kujikinga na V.V.U | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea namna mtoto anavyoweza kujikinga na V.V.U. | 1. Bomba la sindano<br>2. Sindano ya kushonea.<br>3. Kiwembe.<br>4. Kampasi.<br>5. Vitu vyenye ncha kali.<br>6. Mate.<br>7. Mabofu. | |
| 10. USALAMA<br>(a) Utumizi wa | Mtoto aweze: kuelezea namna bora ya utumiaji | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze | 1. Chati inayoonesha mandhari ya barabara, gari, | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Barabara. | wa barabara. | watoto kuelezea namna wanavyotembea barabarani.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kuigiza namna bora ya kutembea barabarani.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza namna ya kuvuka barabara .<br>4. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze wanafunzi kuvuka barabara iliyo karibu | baskeli, Honda na watu wanaotembea kwa miguu. | |
| (b) Mazingira Hatari | Mtoto aweze Kutaja maeneo wanaoweza kuhatarisha usalama wao mfano vichochoroni, vichakani | Kwa kutumia mbinu ya hadithi mwalimu awaongoze watoto kutaja maeneo yanayohatarisha usalama wao. | 1. Chati inayoonesha maeneo ya hatari/chati mguso.<br>2. Chati ya hadithi inayoonesha mazingira ya hatari/chati mguso. | 3 |
| 11. MAJENGO<br>(a) Majengo ya | Mtoto aweze kuelezea majengo ya kijamii | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze | 1. Chati inayoonesha majengo ya kijamii/chati | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Kijamii. | yaliyokaribu na kwao mfano maduka, skuli, chuo, hospitali, msikiti. | watoto kutaja majengo ya kijamii yaliyokaribu na kwao.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya ziara, mwalimu awaongoze watoto kuainisha majengo ya kijamaa yaliyo karibu na skuli yao. | mguso.<br>2. Modeli ya kijiji iliyomo katika maeneo ya darasa. | |
| 11. MIMEA<br>(a) Uotaji wa Mbegu. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kufanya jaribio la uoteshaji wa mbegu. | 1. Kwa kutumia mbinu ya vikundi mwalimu awaongoze watoto kufanya jaribio la uoteshaji wa mbegu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea hatua za utoaji wa mbegu | 1. Mbegu mbali mbali.<br>2. Vikopo.<br>3. Udongo.<br>4. Maji<br>5. Chati inayoonesha hatua za uotaji wa. mbegu/chati mguso | 6 |
| | (ii) Kutaja mahitaji ya mbegu katika kuotesha | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja mahitaji ya mbegu katika kuotesha. | . Mbegu mbali mbali.<br>2. Vikopo.<br>3. Udongo.<br>4. Maji<br>5. Chati inayoonesha hatua za uotaji wa mmea/chati mguso. | |
| | (iii) Kuchora hatua za uotaji wa mbegu. | Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora | 1. Penseli.<br>2. Rangi za penseli | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | hatua za uotaji wa mbegu. | 3. Karatasi.<br>4. Crayons. | |
| 12. MAJI<br>(a) Umuhimu wa Maji. | Mtoto aweze kueleza umuhimu wa maji katika maisha ya binadamu. | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo inayoelezea umuhimu wa maji | Chati inayoonesha umuhimu wa maji/Chati mguso | 3 |
| (b) Maji Safi na Salama. | Mtoto aweze:<br>(i) Kuelezea maana ya maji safi na salama. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongozee watoto kueleza maana ya maji safi na salama.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutoa tofauti ya maji safi na maji machafu. | Chati inayoonesha umuhimu wa maji/Chati mguso | 3 |
| | (ii) Kuelezea umuhimu wa matumizi ya maji safi na salama. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kuangalia namna ya kuchemsha maji.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo ya umuhimu wa kunywa maji safi na salama. | Chati inayoonesha umuhimu wa maji/Chati mguso | |
| 13. MWANGAZ | Mtoto aweze kutaja | Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu | 1. Tochi, mshumaa, kibatari, | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| A NA GIZA.<br>(a) Mwangaza | vyanzo vinavyotoa muangaza visivyo asili. | awaongoze watoto kutaja vitu vinavyotoa mwangaza visivyo asili. | kandili.<br>2. Chati inayoonesha vitu vinavyotoa muangaza/chati mguso. | |
| (b) Giza. | Mtoto aweze kufanya mazoezi yanayosababisha giza | 1. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto kufanya vitendo vitakavyoonesha giza mfano kufumba macho, kufunga madirisha na milango kujifunika blangeti.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kucheza mchezo wa bui. | 1. Kitambaa.<br>2. Blangeti.<br>3. Madirisha na milango. | 2 |
| 14. TEKNOLOJIA<br>(a) Vifaa vya Electroniki. | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja vifaa vya electroniki vilivyomo katika mazingira yao. | Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kutaja vifaa vya electroniki vilivyomo kwenye mazingira yao. | 1. Pasi, redio, friji, TV, simu, rimoti, kalkuleta (kikokotoa), kompyuta, video<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya electroniki/chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kueleza matumizi ya vifaa vya electroniki | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto | 1. Pasi, redio, friji, TV, simu, rimoti, kalculeta | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kuonesha matumizi ya vifaa vya electroniki. | (kikokotoa), kompyuta, video.<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya electroniki/chati mguso. | |
| | (iii) Kuchora vifaa vya electroniki. | Kwa kutumia mbinu mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora picha za vifaa vya electroniki. | 1. Pasi, redio, friji, TV, simu, rimoti, kalkuleta(kikokotoa), kompyuta, video.<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya electroniki/chati mguso. | |

# MWAKA WA PILI

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. FAMILIA<br>(a) Majukumu ya Watu Katika Familia. | Mtoto aweze kutaja kazi zinazofanywa na watu anaokaa nao nyumbani. | 1. Kwa kutumia mbinu ya masuali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja kazi zinazofanywa na watu anaokaa nao nyumbani.<br>2. Kwa kutumia mbinu igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza kazi zinazofanywa na watu wanaokaa nao nyumbani. | Picha inayoonesha shughuli za watu katika familia mfano kupika, kufua, kupiga pasi. | 6 |
| 2. VIUMBE VYENYE UHAI NA VITU VISIVYO NA UHAI<br>(a) Viumbe Vyenye Uhai. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja mifano ya viumbe vyenye uhai. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutaja viumbe vyenye uhai.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kuonesha viumbe vyenye uhai. | 1. Vitu halisi mf. Mti, ng'ombe, punda, farasi, ndege.<br>2. Picha inayoonesha vitu vyenye uhai/chati mguso. .<br>3. Modeli za vitu vyenye uhai | 6 |
| | (ii) Kuchora viumbe vyenye uhai. | Kwa kutumia mbinu mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora viumbe vyenye uhai. | 1. Vitu halisi mf. Mti, ng'ombe, punda, farasi, ndege.<br>2. Picha inayoonesha vitu vyenye uhai/chati mguso.<br>3. Modeli za vitu vyenye uhai. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (b) Vitu Visivyo na Uhai. | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja vitu visivyo na uhai | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutaja vitu visivyo na uhai.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kuonesha vitu visivyo na uhai | 1. Vifaa halisi. Jiwe, kombe, kiti, meza, buku na gari.<br>2. Chati ya vitu visivyo na uhai /Chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kutofautisha vitu vyenye uhai na visivyo na uhai. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutofautisha vitu vyenye uhai na visivyo na uhai. | Chati ya vitu visivyo na uhai/chati mguso. | |
| | (iii) Kuchora vitu visivyo na uhai. | Kwa kutumia mbinu mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora vitu visivyo na uhai. | Chati ya vitu visivyo na uhai/chati mguso. | |
| 2. NGUVU ZA MAUMBILE<br>(a) Nguvu za Kusukuma. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kufanya jaribio la kusukuma vitu vyenye uzito tofauti. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kusukuma vitu vyenye uzito tofauti.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya jaribio mwalimu awaongoze watoto kufanya jaribio la kusukuma vitu vyenye uzito tofauti.<br>3 Kwa kutumia mbinu ya maswali | 1. Vifaa halisi, bero, boksi, pembea.<br>2. Chati inayoonesha mtu anasukuma pembea , rikwama/Chati mguso. | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja nguvu alizotumia kwa kusukuma vitu mbali mbali | | |
| (b) Nguvu za Kuvuta. | Mtoto aweze Kufanya jaribio la kuvuta. | 1. Kwa kutumia mbinu ya jaribio mwalimu awaongoze watoto kufanya jaribio la kuvuta vitu mbali mbali.<br>2. Kwa kutumia mbinu mchezo mwalimu awaongoze watoto kucheza mchezo wa kuvuta kamba kwa uwiano tofauti wa watoto.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza tofauti za nguvu walizotumia kuvutana wakati wa mchezo. | vitu halisi, roda, kamba | 6 |
| 4. HALI YA HEWA<br>(a) Mabadiliko ya Hali ya Hewa. | Mtoto aweze kutaja mabadiliko ya hali ya hewa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja mabadiliko ya hali ya hewa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kumechisha mwalimu awaongoze watoto kumechisha kadi za hali ya | Chati inayoonesha hali ya hewa/Chati mguso. | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | hewa katika chati.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora picha ya hali ya hewa. | | |
| (b) Miongo | Mtoto aweze kutaja majina ya miongo ya Zanzibar. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya miongo iliyomo kwenye picha.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuhusisha picha na miongo iliyopo.<br>3. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuhusisha miezi na miongo.<br>4. Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora miongo ya Zanzibar | Chati inayoonesha hali ya hewa/Chati mguso. | 6 |
| 5. TEKNOLOJIA YA HABARI NA TEKNOLOJIA<br>(a) Vyombo vya Teknolojia ya | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja vyombo vinavyotumika katika teknolojia ya habari na | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja vyombo vinavyotumika katika teknolojia ya habari na mawasiliano. | Vifaa halisi, simu, TV, Redio, Kompyuta, Intaneti. | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Habari na Mawasiliano. | mawasiliano. | | | |
| | (ii) Kuchora vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. | Kwa kutumia mbinu mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. | Vifaa halisi, simu, TV, Redio, Kompyuta, Intaneti. | |
| (b) Matumizi ya Vyombo vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano | Mwanafunzi aweze kutumia vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano.. | Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kutumia vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. | Vifaa halisi, simu, TV, Redio, Kompyuta, Intaneti. | 6 |
| 6. AFYA NA MARADHI.<br>(a) Namna ya Kujikinga na Maradhi. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja sababu zinazosababisha maradhi ya malaria na kuharisha. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja sababu zinazosababisha maradhi ya malaria na kuharisha. | 1. Modeli ya vitu, chandarua, maji safi na salama, maji yasiyochemshwa (machafu) matunda, sabuni, birika, kopo.<br>2. Chati inayoonesha mtoto aliyefunikwa chandaruwa/ chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kujikinga na maradhi ya malaria na kuharisha. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kuonesha picha zinazoonesha mtoto aliyelala kwenye chandarua, Mtoto anaekosha matunda na mtoto | 1. Modeli ya vitu, chandarua, maji safi na salama, maji yasiyochemshwa (machafu) matunda, sabuni, birika, kopo. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | anaenawa mikono kwa sabuni<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora picha zinazoonesha kujikinga na maradhi ya kuharisha na malaria. | 2. Chati mtoto aliyefunikwa chandaruwa/chati mguso inayoonesha | |
| 7. CHAKULA NA LISHE.<br>(a) Kazi za Makundi ya Vyakula. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja majina ya vyakula. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya vyakula. | 1. Vifaa halisi vya makundi ya vyakula<br>2. Chati inayoonesha makundi ya vyakula/Chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kutaja majina ya makundi ya vyakula. | Kwa kutumia mbinu onyesho mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya makundi ya vyakula. | 1. Vifaa halisi vya makundi ya vyakula<br>2. Chati inayoonesha makundi ya vyakula/Chati mguso. | |
| | (iii) Kazi ya makundi ya vyakula, | Kwa kutumia mbinu ya mswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja kazi za makundi ya vyakula. | 1. Vifaa halisi vya makundi ya vyakula<br>2. Chati inayoonesha makundi ya vyakula/Chati mguso. | |
| 8. DAWA ZA KULEVYA | Mtoto aweze kutaja athari za dawa za | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze | 1. Video<br>2. T.V | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (a) Athari za Dawa za Kulevya | kulevya. | watoto kutaja athari za dawa za kulevya.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza namna watakavyojiepusha na vishawishi vya dawa za kulevya. | 3. CD.<br>4. Chati inayoonesha waathirika wa dawa za kulevya/ Chati mguso | |
| 9. UKIMWI<br>(a) Njia za Kujikinga na Maambukizi ya VVU | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja njia za kujikinga na maambukizi ya VVU | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja njia za kujikinga na maambukizi ya VVU | 1. Video<br>2. T.V.<br>3. CD | 6 |
| | (ii) Kutaja mambo anayoweza kushirikiana na mgonjwa wa UKIMWI. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja mambo ambayo wanaweza kushirikiana na wagonjwa wa UKIMWI. | 1. Redio<br>2. T.V.<br>3. CD. | |
| 10. USALAMA<br>(a) Alama za Barabarani. | Mtoto aweze kuzitumia alama za barabarani. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kutaja alama za barabarani (wanazozijua).<br>2. Kwa kutumia mbinu ya ziara mwalimu awapeleke watoto | Chati inayoonesha alama za barabara/Chati mguso. | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | barabarani na awaoneshe alama za barabarani.<br>3. Kwa kutumiia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto kuvuka barabara kwa kutumia alama ya kuvuka barabara. | | |
| (b) Ajali | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja aina za ajali. | 1. Kwa kutumia onyesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja aina za ajali (moto, maji na gari).<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea ajali walizowahi kuziona. | 1. Chati inayoonesha ajali za barabarani.<br>2. Moto<br>3. Maji<br>4. Chati mguso | 3 |
| | (ii) Kujikinga na ajali. | 1. Kwa kutumia onyesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuelezea namna ya kujikinga na ajali..<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza namna watakavyojikinga na ajali ya moto ikitokea darasani. | Kifirimbi kinachoonesha kutokea kwa ajali. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (b) Athari Zinazopatikana Kutokana na Ajali. | Mtoto aweze kueleza athari zinazopatikana kutoka na ajali. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza athari zinazopatikana kutokana na ajali. | 1. Picha inayoonesha watu walioathirika kutokana na ajali.<br>2. Chati mguso. | 3 |
| 11. MAJENGO<br>(a) Majengo ya Kitaifa. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja majengo ya kitaifa. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya majengo ya kitaifa. | 1. Chati inayoonesha majengo ya kitaifa.<br>2. Chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kueleza matumizi ya majengo ya kitaifa, | Kwa kutumia mbinu ya ziara mwalimu awaongoze watoto kueleza matumizi ya majengo ya kitaifa, | 1. Chati inayoonesha majengo ya kitaifa.<br>2. Chati mguso. | |
| | (iii) Kuchora majengo ya kitaifa. | Kwa kutumia mbinu mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora majengo ya kitaifa. | 1. Chati inayoonesha majengo ya kitaifa.<br>2. Chati mguso. | |
| 13. MITI MIKUBWA NA MIDOGO<br>(a) Majina ya Miti. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja majina ya miti. | Kwa kutumia onyesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya miti. | 1. Chati inayoonesha miti mbali mbali/Chati mguso ya miti mbali mbali. | 6 |
| | (ii) Kuainisha sehemu | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho | 1. Chati inayoonesha miti | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | za miti. | mwalimu awaongoze watoto kuainisha sehemu za miti.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya ziara mwalimu awaongoze watoto kuainisha sehemu za miti kwa kutumia miti halisi iliyopo katika eneo la skuli. | mbali mbalichati mguso.<br>2. Chati ya sehemu za miti (kigogo, majani, shina, matawi | |
| | (iii) Kuchora miti. | Kwa kutumia mbinu ya mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora picha za miti. | 1. Chati inayoonesha miti mbali mbali/chati mguso.<br>2. Chati ya sehemu za miti (kigogo, majani, shina, matawi) | |
| 13. MWANGAZA<br>(a) Matumizi ya Vitu Vinavyotoa Mwangaza. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja matumizi ya vitu vinavyotoa mwangaza. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja matumizi ya vitu vinavyotoa mwangaza.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya jaribio mwalimu awaongoze watoto kufanya jaribio la kutumia vitu vinavyotoa mwangaza. | 1. Vitu halisi, moto, kibatari, tochi, mshumaa.<br>2. Chati inayoonehsa vitu vinavyotoa mwangaza/ Chati mguso | 6 |
| | (ii) Kutumia vitu vinavyotoa mwangaza | Kwa kutumia mbinu ya jaribio mwalimu awaongoze watoto kufanya jaribio la kutumia vitu vinavyotoa | 1. Vitu halisi, moto, kibatari, tochi, mshumaa.<br>2. Chati inayoonehsa vitu | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | mwangaza. | vinavyotoa mwangaza/ Chati mguso | |
| | (ii) Kuchora picha ya vitu vinavyotoa mwangaza. | Kwa kutumia mbinu onyesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuchora vitu vinavyotoa mwangaza. | .1. Vitu halisi, moto, kibatari, tochi, mshumaa.<br>2. Chati nayoonehsa vitu vinavyotoa mwangaza/chati mguso. | |
| 14. TEKNOLOJIA<br>(a) Vifaa vya Teknolojia Vinavyotumika Nyumbani. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani.<br>2. Kwa kutumia onyesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuonesha vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani. | 1. Vifaa halisi, redio, pasi, T.V, blenda, friji, feni<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani/Chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kutumia vifaa vya teknolojia vya nyumbani. | Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kutumia vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani. | 1. Vifaa halisi, redio, pasi, T.V, blenda, friji, feni<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya | |
| | | | teknolojia vinavyotumika nyumbani/Chati mguso. | |
| | (iii) Kuchora picha | Kwa kutumia mbinu mchoro mwalimu | 1. Vifaa halisi, redio, pasi, | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | ya vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani. | awaongoze watoto kuchora vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani mfano. Pasi, blenda, friji, T.V. Redio. | T.V, blenda, friji, feni<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani/Chati mguso. | |
| (b) Athari Zinazopatikana na Vifaa vya Teknolojia. | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja athari zinazopatikana kutokana na vifaa vya teknolojia | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja athari zinazopatikana kutokana na vifaa vya teknolojia inayotumika nyumbani | 1. Vifaa halisi, pasi, feni, friji, redio, TV.<br>2. Chati inayoonesha Vifaa vya teknolojia Vinavyotumika nyumbani/chati mguso. | 6 |
| | (ii) Kujikinga na athari za vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kueleza namna ya kujikinga na athari zinazotokana na vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani | 1. Vifaa halisi, pasi, feni, friji, redio, TV<br>2. Chati inayoonesha vifaa vya teknolojia vinavyotumika nyumbani/chati mguso. | |